JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

# MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI

1. Unatakiwa kununua vifaa na mahitaji yafuatayo kwa matumizi yako ukiwa chuoni;-

**A. Sare ya chuo**

(i) Mashati mawili meupe ya mikono mfupi kitambaa cha tetroni.

(ii) Suruali mbili za rangi ya bluu iliyokoza (dark blue). Mfano wa kitambaa umeambatanishwa na fomu hii, utashona kabla ya kuja chuoni kwa vipimo cha upana wa miguuni wa **inchi 18** kwa wavulana na **inchi 17** kwa wasichana.

(iii) Jozi ya **viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi** vitakavyovaliwa wakati wa mafunzo ya nadharia madarasani.

(iv) Jozi ya **viatu vya usalama (Safety Boots)** vitakavyovaliwa wakati wa mafunzo ya vitendo ndani ya karakana za mafunzo.

(v) Ovaroli Moja ya rangi ya bluu iliyokoza ( dark blue).

(vi) Soksi ndefu Jozi mbili za rangi **NYEUSI**.

(vii) **Nguo za michezo** - fulana na Suruali ya ***truck suit*** vya rangi ya bluu na raba nyeusi.

(viii) Sweta ya rangi ya bluu iliyokoza (dark blue).

**B. Vifaa vingine**

(i) Madaftari makubwa manane (8) ya **4Q**

(ii) Daftari Moja la Somo la **Uchoraji Sanifu**. Hili utalitengeneza kwa kutumia karatasi nyeupe za A4 , 200 au zaidi na kuzifunga pamoja kwa ***spriral binding.***

(iii) Seti ya vifaa vya hesabu (Mathematical set).

(iv) Kalamu za wino na penseli(2B na HB) za kutosha

(v) **Fyekeo/Jembe/Reki** kwa ajili ya usafi wa mazingira.

(vi) Rimu moja ya karatasi za A4 aina ya **Nopa** au **Mondi** (*itakabidhiwa ofisini*).

2. Unatakiwa kuja na kiasi cha fedha za kulipia mahitaji yaliyoorodheshwa hapa chini na ufikapo chuoni utapewa namba ya malipo ya serikali (Control number) utalipia na kuwasilisha stakabadhi ya malipo kwenye ofisi ya mhasibu. isipokuwa namba (xi). Hii italipwa mwanafunzi anapokamilisha usajili na control namba itatolewa na mfuko wa bima ya afya (NHIF).

## C.VIGEZO VYA KUPATA BIMA YA AFYA (NHIF) KWA WASIO NA BIMA YA AFYA.

Ili kupata bima ya afya unapaswa kuwa na vigezo vifuatavyo.

i. **Unatakiwa kuja na copy ya cheti cha kuzaliwa**
ii. **Unatakiwa kuja na Copy ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au number ya NIDA.**

**MUHIMU: KUKAMILISHA USAJILI NI LAZIMA UWE NA VIGEZO VYA KUPATA BIMA AU KUWA NA BIMA YA AFYA.**

**JEDWALI A (Control number itatolewa chuoni isipokuwa namba xi)**

| SNO. | AINA YA MALIPO | KIASI (TSHS) | |
|---|---|---|---|
| | | AWAMU YA I | AWAMU YA II |
| i | Ada ya mafunzo (KUTWA) | 30,000/= | 30,000/= |
| ii | Ada ya mafunzo (BWENI) | 60,000/= | 60,000/= |
| iii | Mahafali | 10,000/= | |
| iv | Kitambulisho (ID) | 5,000/= | |
| v | Fulana ya VETA (T-Shirt) | 18,000/= | |
| vi | Nembo (Emblem) | 5,000/= | |
| vii | Fedha ya Ukarabati | 20,000/= | |
| viii | Fedha ya Michezo | 10,000/= | |
| ix | Godoro | 10,000/= | |
| x | Ada ya mtihani (Life Skills) | 25,000/= | |
| xi | Bima ya Afya (NHIF) | 50,400/= | |
| | **JUMLA(KUTWA)** | **173,400/=** | **30,000/=** |
| | **JUMLA(BWENI)** | **213,400/=** | **60,000/=** |

